KUTATHMINI HATUA YA MWANAFUNZI

KAKAMEGA NORTHERN CLUSTER

GREDI 4 - 2020

SHUGHULI ZA KISWAHILI

JINA:.....

JINA LA SHULE:.....

Mwalimu ajaze mjalizo baada ya kusahihisha kazi ya mwanafunzi

	Swali la 1	Swali la 2	Swali la 3	Swali la 4
Idadi ya alama	10	20	5	15
Alama sahihi				

SOMA HADITHI IFUATAYO KISHA UJIBU MASWALI

Musa alifanya ziara ya kumzuru babu yake. Alifika kijijini wakati wa jioni. Babu alimkaribisha Musa kwa furaha tele. Babu alilifungua kufuli lililokuwa kwenye tumbuu. Wote wakaingia sebuleni. Aliuweka mzigo wake kwenye mtoto wa meza. Kwa kuwa mwangaza ulikuwa hafifu , babu alibofya swichi na balbu ikasambaza mwangaza kote chumbani.

Nyanya alimwandalia mjukuu wake chajio mezani. Kwa kuwa baridi ilikuwa imeanza kuingia, babu alimpa koti refu akalivaa. Koti hilo lilikuwa limemfika kwenye goti. Baada ya kufanya maombi na kumsimulia hadithi. Musa alielekezwa kwenye chumba chake cha kulala. Nyanya alifunga neti kwenye fremu iliyokuwa darini kisha akaifunga kwenye tendegu la kitanda. Musa aliingia kitandani na kulala fofofo!